## SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR, NAM. 4 YA 2015

### MPANGILIO WA VIFUNGU


| VIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| | **SEHEMU YA KWANZA** |
| | **MASHARTI YA AWALI** |
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Kusomwa. |
| | **SEHEMU YA PILI** |
| | **MAREKEBISHO YA VIFUNGU MBALI MBALI** |
| 3. | Marekebisho ya kifungu cha 2. |
| 4. | Marekebisho ya kifungu cha 3. |
| 5. | Marekebisho ya Sehemu ya Pili. |
| 6. | Marekebisho ya kifungu cha 4. |
| 7. | Marekebisho ya kifungu cha 5. |
| 8. | Marekebisho ya kifungu cha 6. |
| 9. | Marekebisho ya kifungu cha 9. |
| 10. | Kuongezwa vifungu vipya vya 9A,9B, na 9C. |
| 11. | Kuongezwa kwa vifungu vipya 10A na 10B. |
| 12. | Marekebisho ya kifungu cha 12. |
| 13. | Marekebisho ya kifungu cha 13. |
| 14. | Kuongezwa kifungu kipya cha 16A. |
| 15. | Marekebisho ya kifungu cha 26. |
| 16. | Marekebisho ya kifungu cha 27. |
| 17. | Marekebisho ya kifungu cha 31. |
| 18. | Marekebisho ya kifungu cha 36. |
| 19. | Marekebisho ya kifungu 37. |

**SHERIA NAMBA 4 YA 2017**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

13 Juni, 2017

## SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR, NAM. 4 YA 2015

---

**UMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya (Marekebisho) ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kuwekwa saini na Rais.

Kusomwa.

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Nam. 4 ya 2015, katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA VIFUNGU MBALI MBALI

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**3.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta na kuweka kifungu kipya kama ifuatavyo:

"2. Sheria hii itatumika kwa Viongozi wa Umma kama walivyotafsiriwa katika Sheria hii".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**4.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kufuta na kuweka tafsiri ya maneno yafuatayo:

"mali" maana yake ni kitu, chochote kinachomilikiwa na Kiongozi wa Umma, mume, mke au mtoto wake ambacho kina thamani na kinaweza kuuzwa au kutumika kulipia deni;

"Tume" maana yake ni Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Mgongano wa kimaslahi" maana yake ni hali ambayo Kiongozi wa Umma:

(a) ana maslahi binafsi katika jambo la umma ambalo ana mamlaka nalo; au

(b) anashiriki katika kufanya maamuzi kwa jambo ambalo ana maslahi binafsi;

" Kiongozi wa Umma" maana yake ni mtu yeyote anayeshikilia nafasi ya uongozi wa umma aliyeainishwa au kuorodheshwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

(b) kwa kuongeza katika utaratibu wa mpangilio wa herufi tafsiri mpya ya maneno yafuatayo:

"Taasisi ya Umma" maana yake ni ofisi au taasisi inayojitegemea au isiyojitegemea kikamilifu katika utumishi wa umma;

(c) kwa kufuta tafsiri ya neno "kiongozi" na kuweka badala yake "kiongozi wa umma" popote itakapojitokeza katika Sheria hii;

(d) kwa kufuta tafsiri ya neno "maadili" .

Marekebisho ya Sehemu ya Pili.

**5.** Sheria Mama inarekebishwa katika Kichwa cha Habari cha Sehemu ya Pili kwa kufuta maneno "KANUNI ZA" yanayojitokeza baina ya maneno "VIONGOZI" na "MAADILI".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**6.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "kanuni ya" yanayojitokeza baina ya maneno "viongozi" na "maadili".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**7.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kukipa nambari mpya kifungu cha 5 kuwa kifungu cha 5(1);

(b) kwa kukipa nambari mpya kifungu cha 5(a) kuwa kifungu kidogo cha (2) na kufuta maelezo yake na kuweka maelezo mapya yafuatayo:

"(2) Mwenyekiti atasimamia kazi za Tume na atatekeleza majukumu na mamlaka ya Tume yaliyoainishwa katika Sheria hii."

(c) kwa kukipa nambari mpya kifungu cha 5(b) kuwa kifungu kidogo cha (3);

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**8.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kuyapa nambari maelezo yaliyojitokeza mara baada ya kifungu cha 6(2) kuwa kifungu kidogo kipya cha (3), kufuta neno "kidogo" yaliopo baina ya maneno "kifungu" na "hiki";

(b) kwa kuvipa nambari mpya vifungu vidogo vya (3) na (4) kuwa vifungu vidogo (4) na (5);

(c) kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) kilichopewa nambari mpya na kuweka kifungu kipya kama ifuatavyo:

"(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, utovu wa nidhamu maana yake ni ukiukaji wa miiko ya uongozi kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 18 cha Sheria hii".

(d) kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (5) vifungu vidogo vipya vya (6), (7) na (8) vifuatavyo:

"(6) Endapo Mwenyekiti hatokuwepo Ofisini au atashindwa kutekeleza majukumu yake, Rais anaweza kumteua, kwa kipindi maalum, mtu yeyote kuwa Kaimu Mwenyekiti ambaye atatekeleza majukumu ya Mwenyekiti".

"(7) Mtu yeyote hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Kaimu Mwenyekiti isipokuwa mtu huyo awe na sifa za kuwa Mwenyekiti zilizoainishwa katika kifungu cha 7(1) na (2) cha Sheria hii".

"(8) Mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Mwenyekiti hatoanza kazi mpaka atakapokula kiapo mbele ya Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**9.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kukipa nambari mpya kifungu cha 9 kuwa kifungu cha 9(1);

(b) kwa kuingiza mara baada ya kifungu kidogo kipya cha (1) kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Kamishna atashika nafasi yake kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine."

Kuongeza vifungu vipya vya 9A, 9B na 9C.

**10.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 9, vifungu vipya vya 9A, 9B na 9C kama ifuatavyo:

Kufuta uteuzi wa Kamishna.

"9A. Rais anaweza kufuta uteuzi wa Kamishna, kutokana na:

(a) kushindwa kutekeleza majukumu yake;

(b) utovu wa nidhamu;

(c) kutiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na maadili;

(d) kushindwa kufuata masharti ya Sheria hii; au

(e) sababu nyengine yoyote ya msingi.

Kujiuzulu kwa Kamishna.

"9B.-(1) Kamishna anaweza, wakati wowote, kujiuzulu kwa kumuandikia barua rasmi Rais.

(2) Mtu atasita kuwa Kamishna kuanzia tarehe atakayopokea barua kutoka kwa Rais.

Nafasi ya Kamishna kuwa wazi.

"9C. Nafasi ya Kamishna itakuwa wazi:

(a) kwa kifo, kujiuzulu au kusitishwa uteuzi wa Kamishna; au

(b) kwa kutokuhudhuria vikao vitatu vya Tume kwa mfululizo, isipokuwa kutokuhudhuria huko kumeidhinishwa na Mwenyekiti. au"

(c) kwa kumalizika muda wa utumishi.

Kuongezwa kwa vifungu vipya vya 10A na 10B.

**11.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 10 vifungu vipya vifuatavyo vya 10A na 10B:

Katibu wa Tume.

"10A-(1) Kutakuwa na Katibu wa Tume atakayeteuliwa na Rais.

(2) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Katibu wa Tume isipokuwa mtu huyo awe:

(a) ni Mzanzibari na angalau ana shahada ya Kwanza ya Sheria, Utawala wa Umma, Uongozi au fani nyengine yoyote inayolingana na hizo; na

(b) na uzoefu usiopungua miaka saba katika fani husika; na

(c) mwenye kiwango kikubwa cha uadilifu katika Utumishi wa Umma.

(3) Katibu wa Tume hatoanza kazi hadi ale kiapo mbele ya Rais.

Majukumu ya Katibu.

10B.-(1) Katibu wa Tume, kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii na maelekezo ya Mwenyekiti, atakuwa Afisa Mtendaji wa Tume, na kwa nafasi yake atawajibika kwa Tume kwa kazi za kiutawala za kila siku za Tume.

(2) Pamoja na majukumu yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1), Katibu:

(a) atahudhuria vikao vya Tume;

(b) ataweka kumbukumbu za mikutano ya Tume na kuzihifadhi katika namna muafaka; na

(c) kwa ujumla, atatekeleza kazi nyengine zinazohusiana na majukumu ya Tume kama atakavyoelekezwa na Tume.

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**12.** Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kuingiza mara baada ya kifungu kidogo cha (1) (m) aya mpya (n) kama ifuatavyo:

"(n) kufanya ukaguzi wa moja kwa moja kuhusiana na tamko la mali na madeni lililowasilishwa kwa mujibu wa Sheria hii;"

(b) kuipa nambari mpya aya (n) kuwa aya (o).

Marekebisho ya kifungu cha 13.

**13.** Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya aya (c) aya mpya (d) ifuatayo:

"(d) kumtaka mtu yeyote kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuhojiwa kwa njia ya mazungumzo au maandishi kuhusiana na jambo lolote linaloweza kusaidia katika uchunguzi wa tuhuma za uvunjifu wa Sheria hii."

Kuongezwa kifungu kipya cha 16A.

**14.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 16, kifungu kipya cha 16A kifuatacho:

Maombi ya taarifa za ziada.

"16A-(1) Tume itachambua tamko la mali na madeni lililowasilishwa kwa mujibu wa Sheria hii, na itahakikisha kuwa linakidhi matakwa ya Sheria, na inaweza kumtaka Kiongozi wa Umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni aliloliwasilisha.

(2) Tume inaweza kumtaka:

(a) Kiongozi wa Umma kuwasilisha taarifa kuhusiana na masuala ya fedha au mali zake kama itakavyohitajika; au

(b) Kiongozi wa Umma kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuthibitisha Tamko la Mali na madeni."

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**15.** Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuingiza neno "ama" baina ya maneno "ya" na "wote"; na kuingiza mwisho wa kifungu kidogo hiki maneno "au mtu anayelalamikiwa pekee kama Tume itakavyoamua."

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**16.** Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta maneno " kama hakuna rufaa iliyokatwa" yaliyopo mwisho wa kifungu kidogo hicho.

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**17.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kukiandika upya kama ifuatavyo:

Makosa

" 31. Mtu yeyote, bila ya sababu ya msingi au sababu ya kisheria:

(a) anayemzuia mtu anayetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) anayekataa maelekezo yoyote ya Mwenyekiti kwa mujibu wa Sheria hii;

(c) anayekataa wito wa Tume; au

(d) anayetoa taarifa yoyote aliyoipata katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii.

ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au atatumikia adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili faini na kifungo.

Marekebisho ya kifungu cha 36.

**18.** Kifungu cha 36 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno ya pembeni na kuweka maneno mapya "Taarifa za mwaka wa fedha".

Marekebisho ya kifungu cha 37.

**19.** Kifungu cha 37 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kufuta maneno ya pembeni na kuweka maneno mapya "Ukaguzi wa Akaunti ya Benki";

(b) kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (2), kifungu kidogo kipya cha (3) kifuatacho:

"(3) Katika utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mwenyekiti, kwa amri ya maandishi iliyoambatanishwa na hati iliyotolewa na Hakimu wa Mkoa, atamuidhinisha afisa wa Tume kuchunguza akaunti ya fedha ya Kiongozi wa Umma anayehusika."

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 12 Mei, 2017.

.........................................
RAYA ISSA MSELLEM
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar***